**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Anuani ya simu "ELIMU"
Simu: 026 296 35 33
Baruapepe:info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
**40479 DODOMA.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

**Kumb.Na.CA.229/238/01/52**

**28 Februari 2023**

Mwenyekiti,
TAMONGSCO,
S.L.P 63088,
**DODOMA.**

Katibu Mtendaji,
Christian Social Services Commission (CSSC),
S.L.P 1454,
**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji,
Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA),
S.L.P 21422,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,
Tanzania Association of Private Investors in Education (TAPIE),
S.L.P 13346,
**DAR ES SALAAM.**

Mwenyekiti,

Baraza la Sunnar Tanzania (BASUTA),

S.L.P 8581,

**DAR ES SALAAM.**

Mkurugenzi,

Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET),

S.L.P 13547,

**DAR ES SALAAM.**

**Yah: WARAKA WA ELIMU NA. 02 WA MWAKA 2023 KUHUSU UTOAJI WA HUDUMA YA KULAZA WANAFUNZI BWENI KWA NGAZI ZA ELIMU YA AWALI NA SHULE ZA MSINGI**

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

2. Maendeleo ya kweli katika nchi yoyote ile, kwa kiasi kikubwa, hutegemea ubora wa elimu inayotolewa katika nchi husika. Ingawa dhana ya ubora wa elimu hutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine, katika muktadha wa nchi yetu, elimu bora ni ile inayomjengea mhitimu uwezo wa **kuchambua masuala mbalimbali kwa ufasaha ili kufanya maamuzi yenye tija**, **kuwa na maadili yanayoakisi mila, desturi na tamaduni zetu** pamoja na **kujenga moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi** ili kuleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na Taifa kwa ujumla. Maeneo hayo matatu ni muhimu yazingatiwe katika mchakato wa utoaji wa elimu ili wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu watoe mchango stahiki kwenye harakati za maendeleo nchini.

3. Taarifa mbalimbali zilizopo kutoka kwa Wathibiti Ubora wa Shule na Ufuatiliaji unaofanywa na Wizara kwa ujumla umeonesha kwamba shule nyingi zimetoa kipaumbele katika kuwafanya wanafunzi kupata ufaulu mzuri kwenye mitihani yao ya mwisho. Matokeo yake, kuna juhudi hafifu za kujenga maadili ya wanafunzi na kuwajengea moyo wa kupenda, kuthamini na kufanya kazi. Hali hiyo inaondoa dhana muhimu isemayo kwamba **elimu ni maisha na maisha ni kazi**. Moja ya mikakati inayofanywa na shule hizo ili kuongeza ufaulu ni kupitia uanzishwaji wa huduma za bweni hasa kwa madarasa ya mitihani na madarasa mengine kwa ujumla. Aidha, azma

ya kuongeza ufaulu imedhihirika kwa shule hizo kuanzisha makambi ya kitaaluma ambayo hufanyika wakati wa likizo. Hata hivyo, makambi mengi yamebainika kuwa na mazingira hatarishi kimaadili, usalama na afya za wanafunzi kutokana na kuanzishwa bila kufuata taratibu rasmi za uanzishwaji wa bweni au makazi ya pamoja ya wanafunzi.

4. Kwa upande mwingine, malezi na makuzi ya mtoto yanategemea sana mchango mkubwa unaotolewa na familia kupitia wazazi/walezi wa watoto hao. Hata hivyo, imebainika kuwa kuna baadhi ya shule zimekuwa zikipokea watoto wenye umri mdogo kuanzia darasa la awali hadi darasa la nne. Huduma za bweni kwa wanafunzi wenye umri mdogo ikiwemo wale wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza hadi la Nne huwanyima watoto fursa ya kushikamana na familia na jamii zao, kujenga maadili na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendelo ya familia na jamii zao. Kulingana na tafiti zilizopo, madhara ya muda mrefu yatokanayo na tabia ya kulaza watoto bweni katika umri mdogo ni watoto kukosa mapenzi kwa wazazi/walezi na jamii zao na hivyo kushindwa kuwa sehemu ya familia na jamii husika.

5. Kwa Waraka huu, Wizara inawakumbusha na kuwaagiza wamiliki wote wa shule kutekeleza yafuatayo:

a) Huduma za Bweni zitolewe kuanzia Darasa la Tano na kuendelea. Hairuhusiwi kutoa Huduma ya Bweni kwa Wanafunzi wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza hadi la Nne isipokuwa kwa **Kibali Maalumu** kitakachotolewa na Kamishna wa Elimu baada ya kupokea maombi rasmi kutoka kwa Mdau husika. Hatua hii ni utekelezaji wa **Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule** uliotolewa na Wizara mwezi Novemba, 2020. Shule zote ambazo zinatoa Huduma ya Bweni kwa madarasa yasiyoruhusiwa zinaagizwa kusitisha huduma hiyo ifikapo mwisho wa Muhula wa Kwanza mwaka 2023; na

b) Hairuhusiwi kwa shule yoyote ile kuwa na makambi ya kitaaluma. Hatua hii inaakisi utekelezaji wa **Waraka wa Elimu Na 3 wa Mwaka 2007 kuhusu Kukataza Kambi za Masomo katika Shule za Msingi**. Aidha, shule zote zinaelekezwa kuweka mikakati thabiti ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia Kalenda za Mihula zinazotolewa mara kwa mara na Kamishna wa Elimu ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

6. Ili kuhakikisha kwamba Waraka huu unatekelezwa ipasavyo, kutakuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara kupitia Wathibiti Ubora wa Shule na viongozi mbalimbali wa elimu. Shule itakayobainika kukiuka maelekezo ya Waraka huu itachukuliwa hatua za kinidhamu, kisheria au kufutiwa usajili.

7. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Machi, 2023.

8. Nawatakia utekelezaji fanisi.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule Kanda na Wilaya

**TANZANIA BARA**